



AZIMIO NA. 03/2019

AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA UBADILISHAJI HADHI SEHEMU YA PORI LA AKIBA LA SELOUS KUWA HIFADHI YA TAIFA YA NYERERE

KWA KUWA, Sera ya Wanyamapori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuwai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu;

NA KWA KUWA, Sera ya Utalii ni kukuza uchumi na maisha ya wananchi hasa katika kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii unaojali mazingira na wenye faida kiuchumi;

NA KWA KUWA, Pori la Akiba la Selous lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la Mwaka 1974 ambapo imekusudiwa Tangazo hilo lifutwe ili kubadilisha hadhi ya sehemu ya pori hilo kuwa Hifadhi ya Taifa;

NA KWA KUWA, kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282 kinampa Rais, kwa idhini ya Bunge na kwa Tangazo la Rais litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali, mamlaka ya kutangaza eneo la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa kwa madhumuni ya sheria hiyo;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, ili kuanzisha Hifadhi ya Taifa ni sharti kupata ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA, kubadilisha hadhi ya uhifadhi wa sehemu ya Pori la Akiba Selous lenye ukubwa wa kilomita za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere kutaimarisha uhifadhi wa bioanuwai hususan za wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na hivyo kuongeza utalii wa ndani, kukuza uchumi wa jamii inayozunguka hifadhi, utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea Hifadhi hiyo;

NA KWA KUWA, kwa kuridhia Azimio hili, Taifa litapata manufaa yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine wa kwenye maji; na
- (b) Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa ubadilishaji hadhi wa sehemu ya pori hilo utasababisha hifadhi hiyo kuwa Kivutio cha Utalii.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa ya utangazaji wa Hifadhi tajwa ya Taifa, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Sita na kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282 linaazimia kuridhia Azimio la Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilomita za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere. Hivyo mipaka ya Hifadhi ya Taifa Nyerere itasomeka kama inavyoanishwa katika Kiambatisho cha Azimio hili.

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 09 Septemba, 2019

Stephen Kagaigai
KATIBU WA BUNGE

HIFADHI YA TAIFA YA NYERERE


Mipaka ya Hifadhi ya Taifa NYERERE

Kuanzia (Commencing at)

Beacon	Eastings	Northings	Beacon	Eastings	Northings
NNP-1	401283	9194128	NNP-51	256993	8849827
NNP-2	412895	9189691	NNP-52	254925	8860312
NNP-3	431315	9187712	NNP-53	246686	8866004
NNP-4	435001	9180752	NNP-54	237833	8871447
NNP-5	442710	9174040	NNP-55	228766	8871907
NNP-6	445308	9170762	NNP-56	218218	8873550
NNP-7	436436	9162141	NNP-57	207006	8876597
NNP-8	428414	9154006	NNP-58	200205	8883154
NNP-9	419811	9146276	NNP-59	193865	8893396
NNP-10	415634	9136936	NNP-60	187379	8903231
NNP-11	405945	9137051	NNP-61	182231	8914241
NNP-12	393634	9137283	NNP-62	181584	8926218
NNP-13	381829	9136082	NNP-63	185531	8937286
NNP-14	372338	9130680	NNP-64	184739	8949514
NNP-15	368218	9121939	NNP-65	189431	8959287
NNP-16	361347	9113345	NNP-66	197461	8968077
NNP-17	354219	9104727	NNP-67	204225	8969925
NNP-18	348479	9094081	NNP-68	214756	8969827
NNP-19	339369	9086270	NNP-69	223925	8972293
NNP-20	334048	9076172	NNP-70	233440	8975992
NNP-21	326848	9067335	NNP-71	242285	8983602

Beacon	Eastings	Northings	Beacon	Eastings	Northings
NNP-22	318876	9059514	NNP-72	252873	8990000
NNP-23	320407	9048466	NNP-73	264642	8993803
NNP-24	318057	9038105	NNP-74	269481	9004236
NNP-25	314941	9027502	NNP-75	267842	9016477
NNP-26	311768	9018056	NNP-76	269417	9028724
NNP-27	314725	9008799	NNP-77	266928	9040846
NNP-28	317922	9000837	NNP-78	263275	9052677
NNP-29	320572	8992109	NNP-79	259245	9064416
NNP-30	329140	8987278	NNP-80	259003	9076359
NNP-31	332132	8980612	NNP-81	253974	9087727
NNP-32	328296	8969650	NNP-82	252726	9097432
NNP-33	325531	8958864	NNP-83	262135	9097347
NNP-34	326143	8947703	NNP-84	269559	9103544
NNP-35	327199	8942422	NNP-85	278467	9109153
NNP-36	318813	8943914	NNP-86	277169	9121241
NNP-37	319141	8931497	NNP-87	275156	9133494
NNP-38	320355	8919179	NNP-88	285348	9137472
NNP-39	327700	8910017	NNP-89	296095	9142081
NNP-40	333534	8900381	NNP-90	308257	9143064
NNP-41	334506	8888060	NNP-91	319173	9139581
NNP-42	334906	8878200	NNP-92	328848	9147020
NNP-43	328085	8872539	NNP-93	337705	9155093
NNP-44	319072	8866958	NNP-94	346016	9163591
NNP-45	310324	8859788	NNP-95	355411	9170278

Beacon	Eastings	Northings	Beacon	Eastings	Northings
NNP-46	301534	8853460	NNP-96	366070	9173583
NNP-47	293536	8851804	NNP-97	375199	9178389
NNP-48	284918	8851901	NNP-98	385704	9180881
NNP-49	276889	8851044	NNP-99	396989	9184408
NNP-50	267450	8846014	NNP-100	244684	8981877



Dodoma,
..... Agosti, 2019

HAK
WMU